

## Jiunge nasi

Namna ya kujihusisha nasi!

Tangu 2016, OONI inashirikiana na taasisi nyingi za haki za kidigitali: **ooni.org/partners**

Jiunge nasi kupitia barua pepe, Twitter na Mastodon, na fanya vipimo vya OONI Probe kusaidia kuongeza uwazi wa udhibiti wa mtandao!

@OpenObservatory @ooni

## Wasiliana na OONI

Kwa maswali, tafadhali jisikie huru kuwatafuta wafanyakazi wa OONI kwa kutuma barua pepe kwenda **contact@openobservatory.org**.

Pia unaweza kushiriki mijadala yetu na kuwasiliana na OONI kupitia Slack: **slack.ooni.org**



OONI

OONI ni mradi wa programu usioingiza faida ambao ulianzishwa mwaka 2012 ili kuonyesha udhibiti wa mtandao duniani kote.

Ifahamu OONI: **ooni.org**

OONI

# Kupima na kuchunguza udhibiti wa mtandani kwa kutumia data za OONI



## OONI | Probe

**OONI Probe** ni programu huru na ya wazi ambayo hufanya vipimo tofauti vya mtandao ili kuangalia yafuatayo:

1. Udhibiti wa tovuti
2. Udhibiti wa app za ujumbe wa papo kwa papo kama vile WhatsApp, Facebook, Signal na Telegram
3. Uzuiaji wa vikwepa udhibiti
4. Kasi na utendaji kazi wa mtandao wako
5. Uwepo wa middleboxes

Pata **OONI Probe** kwenye simu au kompyuta

Sakinisha OONI Probe →

Ili kuchangia vipimo kila siku, wezesha **upimaji wa mojakwamoja** kupitia mpangilio wa programu ya OONI Probe.

Hii itasaidia jumuiya ya uhuru wa mtandao kuona na kuchukua hatua dhidi ya matukio ya udhibiti!










## Zingatia!

Tafadhali **zima VPN yako** unapofanya vipimo ili kupata matokeo ya vipimo sahihi.

**Angalizo:**
Kutumia OONI Probe **kunaweza kuwa hatari** kwa baadhi ya nchi.

Jifunze zaidi:

Mara tu baada ya kutumia OONI Probe, utapata majibu ya vipimo katika programu ya OONI.

Pamoja na taarifa fupi ya matokeo ya vipimo, (mfano tovuti iliyopimwa imedhibitiwa) utapata data za vipimo ambavyo bado havijachakatwa. Matokeo ya vipimo vyako yatachapishwa kama data za wazi muda huohuo.







## OONI | Explorer

Mojakwamoja, matokeo yote ya vipimo huchapishwa kama data za wazi katika OONI Explore: **chanzo kikubwa cha data za udhibiti wa mtandao duniani**.

Tangu mwaka 2012 hadi sasa, data za OONI zimejumuisha **zaidi ya vipimo vya mtandao bilioni vilivyokusanywa kutoka nchi 241**. Kila dakika vipimo vipya huchapishwa ulimwenguni, zikiangazia udhibiti wa mtandao.




**OONI Explorer** ni jukwaa la kimtandao ambalo linakuwezesha kupata vipimo vya OONI vilivyokusanywa duniani kote.

Jifunze zaidi:

Kifaa tafute cha OONI Explorer kinakuwezeshakugundua moja kwa moja **tovuti zilizothibitika kuzuiliwa** ulimwenguni, na kuonyesha data kwa kuzingatia vigezo vingi (mfano. safu ya tarehe, nchi, mtandao, vipimo vya OONI Probe, Kikoa, aina ya tovuti).